Maisha Yaliyojaa Maombi

(A Prayer-Filled Life)

na

Terry Warford

Maisha Yaliyojaa Maombi

(A Prayer-Filled Life)

na

Terry Warford

Nov 5, 2011

Maisha Yaliyojaa Maombi

Sura ya nne nay a tano ya kitabu cha Ufunuo ni vifungu vinavyovutia. Sura ya kwanza inaanza kwa mlango kufunguliwa Mbinguni kwa ajili ya Yohana kuona, na inaendelea kutupa picha ya ibada zinazoendelea Mbinguni. Tunapofika sehem ya katikati ya sura ya tano tunawaona wanyama wanne na wazee ishirini na wanne wakimsifu Yesu kwa ajili ya kuzifia dhambi zetu. walioungana nao ni takribani malaika **MILIONI 102** . Alafu wanaoungana nao ni KILA kiumbe waliopo angani, nchi kavu, chini ya ardhi, na majini.

Mara kabla ya ibada hii ya kushangaza kuanza, maandiko yanaonyesha kitu tunachokifanya kama Wakristo hapa duniani ambayo inaleta furaha kwa Mungu Mbinguni.

Ufu. 5:8, "*Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu.*"

Hivyo, maombi yetu, ni muhim kwa Mungu,. Ni maalum kwake, na anapata furaha kwetu tunapoomba. Zab. 147:11, "*BWANA huwaridhia wao wamchao, na kuzitarajia fadhili zake.*" Hiyo ni hakika ndio tunachofanya wakati tunapoomba.

Mungu aanataka kubariki maombi yetu. 1 Pet. 3:12, "*Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake husikiliza maombi yao; bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.*"

Hebu tujaze maisha yetu kwa maombi. 1 Thes. 5:16-18, "*Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu.*" Kama tukigeukia mfano wa kadhi asiye haki katika Luka 18:1-8, tunaona kwamba kuomba bila kukoma inamanisha kuendele kuja kwa Mungu kwa maombi.

Katika somo hili tutaangalia baadhi ya njia tofauti ambazo zinaweza kusaidia tukajaza maisha yetu kwa maombi, alafu katika jarida lifuatalo uone baadhi ya vitu ambavyo tunataka kujazia maisha yetu.

Maisha yaliyojaa maombi huanza na siku iliyojaa maombi. Ukifikiria kwamba maombi ni moja ya njiaa binafsi ambayo tunaweza kumtukuza Mungu, geukia Zab. 145:2, "*kila siku nitakuhimidi, nitalisifu jina lako milele na milele.*" Hatuhitaji tu kuomba kila siku lakini JAZA kila siku na maombi. Zab. 113: 3, " *Toka maawio ya jua hata machweo yake jina la BWANA husifiwa.*"

Tuanze siku yetu kwa maombi. Zab. 5:3, "*BWANA asubuhi utaisikia sauti yangu, asubuhi nitakungia dua yangu nakutazamia.*"

Mshukuru Mungu kwa kila mlo. 1 Tim. 4:4-5, "*Kwa maana kila kiumbe cha Mungu ni kizuri, wala hakuna cha kukataliwa, kama kikipokewa kwa shukurani; kwa kuwa kimetakwaswa kwa neno la Mungu na kwa kuomba.*"

Mungu kila wakati yupo kwa ajili yako kila unapomhitaji. Zab. 46:1, "*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.*"

Hebu tuwe hara katika kumshukuru na kumsifu. Efe. 5:20, "*Na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Muombe Mungu abariki shughuli zako za kila siku, kama kazi, kazi za shuleni, kazi za kifamilia, kusoma na kujifunza neno lake, kazi nzuri katika huduma yake, n.k. Kol 3:17, "*Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.*"

Mara zote tunatumia kifungu hiki kuonyesha kwamba tunapaswa kufanya vitu vyote kwa mamlaka ya Kristo Yesu, na hakika ndio matumizi ya msitari huu. Lakini tukizingatia kwamba tunaomba kwa jina lake, na msitari pia unazungumzia kutoa shukurani kwa Mungu kwa yeye, tunaweza kuona kwamba msitari huu unahusiana na maombi pia.

Kila siku chukua muda wewe na Mungu peke yenu. Katika Zab. 46:10 Mungu anatuambia, "*Acheni mjue ya kuwa mimi ni Mungu, nitakuzwa katika mataifa, nitakuzwa katika nchi.*" Na msitari wa 11 inatukumbusha, "*BWANA wa majeshi yu pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.*"

Maliza kila siku kwa kuomba. Zab. 92:1-2, "*Ni neno jema <u>kumshukuru</u> BWANA, na kuliimbia jina lako, Ee uliye juu. Kuzitangaza rehema zako asubuhi, na uaminifu wako <u>wakati wa usiku</u>.*"

Hii siyo kusema kwamba hatufanyi chochote bali kuomba kila siku. Nimegundua kuna watu waliotingwa na shughuli huko nje. Mimi ni mmoja wao. Lakini kadiri tunapomhusisha Mungu katika maisha yetu kupitia maombi, ndivyo tunavyoona uzalishaji na kila siku ya furaha katika huduma yake.

Kwa nyongeza katika maombi ya kila siku, kuna njia zingine tunazoweza kujaza maisha yetu kwa maombi.

Kwa kitu kimoja tuna tumaini na malengo ya vitu tunavyovihitaji kutimiza. Mpe Mungu haya kwa njia ya maombi.

Angalia Zab. 37:4, "*Nawe utajifurahisha kwa BWANA , naye atakupa haja za moyo wako.*" Msitari huu unauliza swali. Matakwa yetu ni nini? Jibu liko katika sehemu ya kwanza ya msitari huu, , kuonekana katika

Bwana. Mit. 11:23, "*Haja ya mwenye haki ni mema tu; bali kutaraji kwake mtu mwovu ni ghadhabu.*"

Alafu katika 1 Yoh. 5:14-15 tunaona kwamba tunahitajika kumpa Mungu matakwa yetu katika mapenzi yake, "*Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, tunajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*"

Tunafuatalia ndoto zetu na malengo kwa maamzi na matendo. Tunapaswa kukabidhi haya katika mapenzi ya Mungu pia. Yak. 4:13-15, "*Haya basi ninyi msemao leo au kesho tutaingia katika mji fulani na kuka humo mwaka mzima, na kufanya biashara na kupata faida; walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka. Badala ya kusema, Bwana akipenda tutakuwa hai na kufanya hivi na hivi.*"

Sawa, kuna njia zingine nyingi tunazoweza kujaza maisha yetu kwa maombi. Hapa kuna mapendekezo machache.

Kufunga na kuomba, maombi ya familia, maombi katika ibada, nyakati maalum kwa wewe tu na Mungu katika maombi. Tunaweza kuendelea na kuendelea. Labda una njia nyingine ya maombi maalum ambayo hata sijaifikiria.

Wazo ni kujaza maisha yetu kwa maombi. Maisha yaliyo-JAA maombi yatatusaidia kuwa na nguvu, yatatusaidia kutumika zaidi, Wakristo walio hai, na itatuleta karibu na Mungu.

Yak. 4:8, "*Mkaribieni Mungu naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu enyi wenye nia mbili.*"

Zab. 141:2, "*Sala yangu ipae mbele zako kama uvumba, kuinuliwa mikono yangu kama dhabihu ya jioni.*"

Hapo juu, tumeonyesha baadhi ya njia ambazo tunaweza kujaza maisha yetu na maombi. Sasa tutaangalia baadhi ya vitu tunavyohitaji ili kuweza kujaza maombi yetu. Tutasisitiza ukweli kwamba Mungu anataka na atajibu maombi yetu.

Kwanza kabisa, tunatakiwa kujaza kila maombi na uvumilivu. Na tutavunja uvumilivu huu katika sehemu mbili: tukitambua kwamba mamlaka ya Mungu na kujinyenyekeza wenyewe mbele yake.

Tunapaswa kutambua sehem ya Mungu na mamlaka. Na anatawala mbinguni, tunapaswa kumwacha akatawala maisha yetu. Kwanza, yeye ndiye aliye na malaika 100,000,000 wakimwabudu.

Wakati Yesu alipokuwa anawafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba katika hotuba ya mlimani, hii ilikuwa kanuni ya kwanza aliyowafundisha. Angalia Mat. 6:9, "*Basi ninyi salini hivi, Baba yetu uliye*

mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje." Angalia, siyo kwamba tunapaswa kusema maneno sawa kama alivyosema. Tunapaswa kuomba kwa utaratibu huo. Tukitambua kwamba Mungu ni Baba yetu, kwamba yuko mbinguni, na kwamba jina lake lazima liwe na sehemu ya juu katika mioyo yetu.

Sehemu ya pili ya uvumilivu katika maombi yoyote ni kunyenyekea mbele za Mungu. Hatulingani na Mungu kuweza kuongelewa pasipo nidhamu. Yeye sio "jamaa" kuweza kuchezewa, yeye sio mtumishi wetu kuweza kuagizwa. Yeye ni Baba yetu wa mbinguni, muumba wetu, Mungu wetu. Tunakaribia kiti chake cha enzi tukitarajia rehema zake. Na tunapaswa kufanya hivyo tukiwa tumejinyenyekeza. 1 Pet. 5:6, "*Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake*."

Kwa ukaribu inayohusiana na uvumilivu ni kujaza kila maombi kwa kutoa shukurani.

Soma sura ya kwanza ya Warumi wakati fulani. Uangalie maovu yote katika sehemu ya mwisho ya sura hii: usodoma, mauwaji, uchafu, ukaidi (wasiosamehe), wasiowatii wazazi wao na mambo mengi maovu. Yote haya yalianzia wapi? Angalia msitari wa 21, "*Kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza.*" Hivyo nashawishika kwamba moyo wa shukurani ni ule ulio na mtazamo thabiti tunaouhitaji kama Wakristo. Na moja ya njia tunayoweza kuonyesha shukurani zetu kwa Mungu ni kupitia maombi.

Zab. 100:3-5, "*Jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; nyuani mwake kwa kusifu; mshukuruni, lihimidini jina lake; kwa kuwa BWANA ndiye mwema;rehema zake ni za milele; na uaminifu wake vizazi na vizazi.*"

Kila maombi tuyaombayo lazima yawe na imani. Kuna kanuni mbili za maombi yaliyofundishwa katika 1 Yoh. 5:14-15. Kwanza, katika maombi yetu tunayaweka katika mapenzi ya Mungu. Hiyo ni sehemu ya unyenyekevu. Kanuni ya pili ni imani. "*Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.*"

Kufanya mahitaji yetu. Kuwa wazi. Tumwombe Mungu abariki mahitaji yetu, (kama ziko sawasawa na mapenzi yake). Kila maombi haina maana kwamba inapaswa kuwa na hitaji, lakini maombi mengi yanayo. Fili. 4:6, "

Fuatilia. Maombi mengi ni kwamba tunabadilisha mahitaji yetu kwa Mungu. Lakini ni lini na wapi tunaweza kuzifuatilia, tunapaswa.

Kwa mfano, kama tunaomba kwa majibu kwenye swali, majibu hayo yanaweza kuwa katika Biblia. Chunguza maandiko kupata majibu. Endelea mbele na uombe kwa ajili ya kupata majibu pia, lakini fuatilia maombi hayo kwa kumwuliza Mungu abariki kujifunza kwetu maandiko. Angalia aina hii ya maombi imeandikwa katika Zab. 119:12, "Baadhi ya maombi yanahitaji tendo la ufuatiliaji. Geukia Mat. 7:11-12, "*Ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliyembinguni atawapa mema wao wamwombao? Basi yoyote mtakayo mtendewe na watu nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii.*"

Angalia neno "basi". Yesu anaunganisha kanuni ya Mungu kutubariki na vitu vizuri kama tukimwomba kwa kanuni ya kuwafanyia wengine mazuri. Fuatilia mamombi yetu kwa matendo mema.

Hii ni muhimu. Tunafikiri kwamba Mungu anabariki maombi yetu. Pia tunapaswa kukumbuka kwamba anabariki kazi zetu pia. Yak. 1:25, "*Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo na uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

Kitu kingine cha kufatilia ni kuweka vitu vibaya mbali na maombi yako. Tusichafue mambi yetu kwa ukaidi, uongo au tamaa. Yak. 4:3 inatuonya kwamba Mungu hatayajibu maombi haya, "*Hata mwaomba wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya.*"hakika, tuyaweke haya yote mbali na maisha yetu. (Maombi yanasaidia.)

Kujaza maombi yetu na uaminifu. Kila maombi tunayoomba lazima yawe ya uaminifu. Iwe binafsi au ya watu wengi kama katika ibada au sherehe za harusi, kila maombi lazima yawe ya kweli, lazima yawe ya uaminifu.

Tusome yak. 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.*"

Neno "kwafaa" hapa inasisitiza uaminifu. Andiko hili pia linatengeneza jambo la msingi kwamba wakati mwingine tunapomba na Wakristo wenzetu.

Pia ni muhim wakati mwingine kuomba ukiwa pekee yako. Nenda kwenye Mat. 14:22-23, "*Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande chomboni na kutangulia mbele yake kwenda ng'ambo, wakati yeye alipokuwa akiwaaga makutano. Naye alipokwisha kuwaaga makutano alipanda mlimani faraghani, kwenda kuomba. Na kulipokuwako jioni alikuwako huko peke yake.*" Ndugu na dada, kama Yesu alihisi kwamba anahitaaji muda bora peke yake na Mungu, ni muhim kwetu sisi pia.

Tukumbuke kwa karibu kwamba Mungu anataka ku, anafanya, na atajibu maombi yetu yakiwa sawasawa na mapenzi yake.

Mungu anatubariki kila ssiku. Zab. 68:19, "*Na ahimidiwe Bwana siku kwa siku hutuchukulia mzigo wetu; Mungu ndiye wokovu wetu.*"

Atajibu maombi yetu, kama sisi ni wake. Yesu alisema katika Yoh. 15:7, "*Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.*"

Kwa upendo wa Kristo,

Ndg. Terry Warford